REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 12th March, 2024

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

NOTICES OF MOTIONS

DESILTING OF DAMS IN LAIKIPIA COUNTY

Hon. Salim Edung: Thank you Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT, AWARE THAT water and sanitation services is a function of the County Government as stipulated in part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010;

FURTHER AWARE THAT water is life;

COGNIZANT OF THE FACT that rain water is seasonal;

FURTHER COGNIZANT that a lot of water is lost due to poor water harvesting techniques during the rainy season;

CONCERNED THAT during the dry season, farmers experience low farm productivity due to lack of adequate water to irrigate their lands and water for their livestock causing farmers to incur huge losses;

APPRECIATING THAT dams are ideal for conservation of water during the rainy season for use in the dry season;

NOTING THAT the existing dams are heavily silted thereby reducing their water holding capacity;

This House URGES the County Government to desilt the existing dams across the County in order to restore water storage capacity, prevent flooding during heavy rains, ensure constant water supply for agriculture, mitigate soil erosion and support sustainable development by safeguarding water resources for communities and ecosystems.

ALLOCATION OF OPPORTUNITIES TO LOCALS IN AFFORDABLE HOUSING PROJECT

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you Mr. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

THAT, AWARE THAT Article 43(1b) of the Constitution of Kenya 2010 provides that every person has the right to accessible and adequate housing;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

FURTHER AWARE THAT County Planning and Development including housing is a function of the County Government as stipulated in part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010;

NOTING THAT Housing affordability is a major challenge in Kenya, and many people cannot afford to buy or build their own homes;

COGNIZANT OF THE current affordable housing project in Nanyuki, Laikipia East Sub-County, Laikipia County comprising of 60 studio units, 20 one-bedroom units, 100 two-bedroom units, and 20 three-bedroom units;

CONCERNED THAT there is expected to be an increase in the demand of various building materials and the Government is committed to sourcing this through local supplies;

FURTHER CONCERNED THAT Micro Small and Medium Enterprises (MSMEs) and Jua Kali Artisans are a key part of this local supplies;

This House URGES the County Government to ensure that the residents of Laikipia become the first beneficiaries to be allocated the said housing units and ensure that the local manufacturers and Jua kali industries benefit in provision of building materials and other allied accessories.

MOTION

ALLOCATION OF OPPORTUNITIES TO LOCALS IN AFFORDABLE HOUSING PROJECT

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you Mr. Speaker. I beg to move the following motion;

THAT, AWARE THAT Article 43(1b) of the Constitution of Kenya 2010 provides that every person has the right to accessible and adequate housing;

FURTHER AWARE THAT County Planning and Development including housing is a function of the County Government as stipulated in part 2 of the Fourth Schedule of the Constitution of Kenya, 2010;

NOTING THAT Housing affordability is a major challenge in Kenya, and many people cannot afford to buy or build their own homes;

COGNIZANT OF THE current affordable housing project in Nanyuki, Laikipia East Sub-County, Laikipia County comprising of 60 studio units, 20 one-bedroom units, 100 two-bedroom units, and 20 three-bedroom units;

CONCERNED THAT there is expected to be an increase in the demand of various building materials and the Government is committed to sourcing this through local supplies;

FURTHER CONCERNED THAT Micro Small and Medium Enterprises (MSMEs) and Jua Kali Artisans are a key part of this local supplies;

This House URGES the County Government to ensure that the residents of Laikipia become the first beneficiaries to be allocated the said housing units and ensure that the local manufacturers and Jua kali industries benefit in provision of building materials and other allied accessories.

Bwana Spika, kuhusu huu mswada ni kwamba nyumba ni kitu muhimu katika maisha ya mwanadamu. Tunaelewa na tunajua ya kwamba serikali kuu na katika chama kinachotawala

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

cha UDA katika *manifesto* yake inasema tutakuwa na huu mradi wa nyumba. Haya mambo ya nyumba za bei nafuu ni ajenda ambayo ni ya kusukuma taifa letu na kuhakikisha wananchi wetu wako na nyumba za kuishi.

Katiba inasema kila mtu yuko na haki ya kuwa na nyumba. Serikali kupitia hili jambo inajenga manyumba kila mahali katika nchi hii ya Kenya. Katika Kaunti yetu ya Laikipia, kuna nyumba zinaendelea kujengwa. Kama mwakilishi wa Thingithu ambapo hizi nyumba zinajengwa, langu ni kuhakikisha kwamba nimetetea wananchi walioko sehemu hio na kwamba ile kazi inafanywa mahali pale wapewe nafasi ya kufanya kazi katika huo mradi.

Bwana Spika, huu ni mradi wa mabilioni ya pesa ambazo mwananchi wa kawaida amechangia kwa kutoa ushuru kuhakikisha serikali iko na pesa ya kutosha. Sisi kama wananchi tunapotoa pesa zinaporudi zinafaa kurudi kwetu. Isiwe zinarudi kwa watu fulani ama mabwanyenye fulani kisha tunaacha mama mboga kwa shida. Ukienda kwa ule mjengo, utapata kuna wale wanasukuma *wheelbarrow* ambayo tulikuwa tunafanyia kampeni nayo. Jambo la kushangaza yule anasukuma ile *wheelbarrow* hata sio mtu wa hapa karibu. Kuna ile nyumba inajengwa Meru. Wale wako Meru wapewe. Zile ziko Thingithu na Laikipia Mashariki tunataka kuona watu wa eneo hili wakifanya ile kazi.

Nikiingia hapa nipate mtu kutoka Umande na Tigithi, nitafurahia kwa sababu sote tuko Mashariki mwa Laikipia. Hizi nyumba zinajengwa katika Mashariki mwa Laikipia. Ikiwa tutapata mtu kutoka Magharibi mwa Mukogodo ambapo ni karibu na hapa, bado ni wananchi wetu wanasaidika. Bwana Spika, kumbuka Katiba inaruhusu idadi ya asilimia thelathini kutoka nje. Kwa hivyo, nikikuta watu wawili wametoka Kisumu, sitakuwa na shida kwa sababu nitajua wako katikati ya lengo la Katiba ya asilimia thelathini kwamba ni lazima watoke nje ya Kaunti.

Itakuwa ni jambo la kuhuzunisha ukiingia pale, ukute asilimia themanini ya watu ambao wanafanya kazi hapo si wa hapa. Bwana Spika, unapata mwingine si Mkenya ilhali anafanya kazi hapo. Hata kama ni Mkandarasi, Taifa la Kenya liko na makandarasi ambao wamehitimu. Tuko na watu ambao wanaelewa kufanya hiyo kazi vizuri. Haitakuwa jambo la busara kama tutaruhusu watu watoke mbali, waje wafanye kazi hapa kisha hizo pesa zote ambazo ninatoa pamoja na mama mboga na watu wa bodaboda inaelekea China. Hatutakuwa tunafanyia wananchi wetu wa Laikipia haki.

Bwana Spika, wakati hizo nyumba zitaisha, tunataka kuona watu ambao wako hapa ndio wanapata nyumba. Yule mtu ambaye yuko Nyahururu na Sosian akipata Nyumba hapa, ni wa Laikipia lakini haitakuwa ni jambo la busara ukiingia pale na kukuta yule ambaye amepata nyumba ametoka Mombasa, Kakamega na Wajir ilhali, hapa kwetu wananchi wetu hawana nyumba za heshima. Ukiingia hapa Majengo upate mahali watu wanalala, akiwa ndani ni kama yuko nje. Ukiwa nje unamuona akilala na akiamka.

Tunasikia aibu kwamba wananchi wetu hawana nyumba nzuri. Katika Kijiji cha Likii, unakuta watu wanakaa mahali ng'ombe, kondoo na wanyama wengine wanafaa kukaa. Kwa sababu ya shida katika nchi hii, mwananchi wa kawaida anakaa hapo. Katika vijiji zote kama Maina, unakuta wananchi wako na mazingira duni. Tunajenga Nyahururu na watu ambao wako katika Kijiji cha Maina wawe wa kwanza kupata hizo nyumba. Ni heri wapatiwe kisha serikali ijue vile itadai hizo pesa.

Tuko na jukumu la kuhakikisha wananchi wetu wamepata nyumba za heshima. Bwana Spika, wewe ni Spika wa Kaunti ya Laikipia na tunakuheshimu. Kwa sababu wewe ni binadamu, itakuwa ni jambo la kuhuzunisha kama nitakukuta tukikutafutia nyumba Majengo ilhali wewe ni Spika. Ndio maana Bunge imetafuta nyumba nzuri ya kulingana na heshima yako huko Muthaiga. Hiyo inakubalika kwa Katiba. Vilevile tunataka kuheshimu mwananchi

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

ambaye alinipigia kura. Anaamka saa kumi na mbili kupanga laini hadi mwisho wa lami ili anipigie kura.

Huyu ndiye ameniajiri na itakuwa ni jambo la busara nikisimama hapa kumtetea ili apate nyumba ambazo zinajengwa. Bwana Spika...

Speaker: Order Hon. Stephen! Hon. Wachuka has a matter. Kindly take your seat.

Hon. Irene Wachuka: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Ningemweleza Mheshimiwa Ndiritu kwamba watu wa Majengo ni watu wetu. Sisi pia tumetoka Majengo na akisema watu wa Majengo sio Wakenya, hao ni watu wa Kenya. Ningetaka kumjulisha ya kwamba wale watu ambao wako Majengo, sisi pia tulitoka Majengo na Mungu akatuinua. Asante, Bwana Spika.

Speaker: Thank you, Hon. Irene. Hon. Stephen, you may proceed.

Hon. Stephen Ndiritu: Bwana Spika, nitaeleza mama yao polepole kwa sababu naheshimu umri na miaka yake. Vilevile Bwana Spika, ninajua mama yao hakuelewa ni nini naongea kuhusu Majengo...

Speaker: Hon. Stephen, we are having Hon. Irene Wachuka. Who is mama yao?

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika kwa kunikosoa. Tumezoea kumuita Mheshimiwa Irene Wachuka kama mama yao. Kwa hivyo Bwana Spika, naongea kuhusu Irene Wachuka John ambaye anawakilisha Wadi ya Igwamiti. Namfahamisha ya kwamba nimesema watu ambao wako Majengo wanafaa kukaa kwa nyumba nzuri. Mahali wanakaa ni duni. Najua anajua kuna watu wako katika Kijiji cha Maina na akiulizwa, angependa kuwa na nyumba za mawe ambazo ziko na vigae, stima na televisheni.

Naheshimu watu wa Majengo na ninapoongea hapa nimetoka Majengo na nimeishi huko kwa miaka mingi. Kitambulisho changu kinasoma Majengo. Kwa hivyo, ukiitishwa mtu wa Majengo, itakuwa ni mimi na tunaheshimu watu wa Majengo. Bwana Spika, nyumba ambazo tunaishi si nyumba ambazo zinapendeza. Hatuishi huko kwa sababu tunapenda. Serikali ikiweza kuingilia kati itutengenezee nyumba ama tupatie watu wa Majengo nyumba ambazo zinajengwa hapa ili wapate kuishi katika nyumba nzuri, tutakuwa tumewafanyia haki.

Bwana Spika, nafikiria Mheshimiwa Irene Wachuka anakubaliana na mimi kwamba watu ambao wako Majengo na Kijiji cha Maina wanahitaji kukaa kwenye nyumba nzuri. Ninajua ameridhika kwa sababu ya vile anacheka. Bwana Spika, nilikuwa nasema ya kwamba ni vizuri tuheshimu binadamu. Yule ambaye anaishi katika hizo nyumba, kama sisi viongozi tutakuwa na namna ya kuhakikisha ya kwamba tumeinua maisha ya hawa watu kwa kukaa nyumba za kupendeza, hilo ndilo jambo ambalo tutakuwa tumefanya la busara kama viongozi ambao walipigiwa kura.

Yule mtu ambaye yuko Kijiji cha Maina na Likii ambaye aliamka saa tisa kupanga laini ili anipigie kura pamoja na wengine ambao wako hapa, ni ili sisi tukipata viti, yeye atatengenezewa maisha pamoja na mazingara ambayo anaishi. Ndio maana tunapeleka lami. Saa hii Serikali ya Daktari William Samoei Ruto inaweka lami katika Kijiji cha Maina na ninajua kwamba huo mpango uko na Mheshimiwa Wachuka ni shahidi.

Ninajua tunaweka lami Majengo mahali ambapo mimi nimetoka ili tujaribu kuinua hadhi ya mwananchi ambaye anaishi Majengo. Tunajaribu kutengeneza mitaro ya takataka ambayo inaleta maji machafu ili tuweze kuondoa aibu ya mwananchi ambaye anakaa hapo ambaye aliamka kutupigia kura. Tukisema ya kwamba tunainua maisha ya yule alinipigia kura, mpaka yule ambaye alipigia mpinzani wangu ninampatia nafasi ya kumtengezea.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Kwa sasa tunaongea kuhusu *affordable housing* ambayo ni *Manifesto* ya Chama cha UDA. Katika Bunge hili kuna watu ambao walikuwa katika Chama cha Azimio ambao pia tunapotengeneza hizo nyumba, watakaa huko. Ninajua katika *Manifesto* yao, kulikuwa na agenda ya nyumba. Hata ukisikia wakipiga makelele, tunaongeza nyumba. Bwana Spika, ni vile tu wako upinzani na ni haki yao kupinga lakini hayo yote yako kwenye agenda.

Bwana Spika, naomba Waheshimiwa walio hapa wahakikishe wananchi wamepata nyumba za heshima. Nitasikia aibu kama hizi nyumba zitamalizika kisha nipate watu ambao wako huko ni wa kutoka mbali na Kaunti hii. Kama kuna watu watatoka mbali waje hapa, itabidi tufunge hiyo nyumba mpaka wale watu ambao wako Laikipia wapate nyumba. Sisi ni viongozi na tuko na haki ya kuhakikisha ya kwamba watu wetu wamepata.

Sisi tuko na haki ya kutetea watu wetu ambao walituchagua. Natahadharisha Bunge hili ili tuungane. Hizi nyumba ziko karibu kuisha. Kwa sasa, tunaelekea ghorofa ya tatu na ni lazima tuhakikishe ya kwamba wanaoleta vifaa vya ujenzi kama mchanga, wanatoka Doldol. Tunataka pesa iwachwe Doldol. Tunataka kuona Mheshimiwa Leshuel akileta watu kutoka Mashariki na Magharibi mwa Mukogodo na Sosian ili walete mchanga ili waweze kupata fedha.

Tunataka kuona wale watu ambao wanauza saruji wako na maduka hapa haswa yule ambaye anauza saruji ishirini. Serikali inafaa kuingia hapo na kumnunulia. Sisi tunasema *bottom up* ambayo ni kuinua yule mtu ambaye yuko huku chini na kumleta juu. Ninataka kusisitiza ya kwamba wakati tunaendelea kujenga hizo nyumba, tuhakikishe ya kwamba tumesaidia watu wetu wa *Juakali*.

Kama tunatengeneza kifuli za kufunga nyumba, tunataka kuona zinanunuliwa kwa watu wa soko za *Juakali*. Tunataka kuona wakipata nafasi ya kuuza hapo. Huu ndio wakati ambapo tunataka kuona serikali ikisaidia wananchi wetu. Hilo litafanyika kama viongozi ambao walipigiwa kura wataongozwa na wewe Mheshimiwa Spika. Bwana Spika, ile kura umekalia hapo iko na mwananchi.

Yule ambaye alikuweka hapo alipatiwa kura na watu. Alikuja na kukupatia nguvu ya huyo mwananchi kwa kukupatia kura. Pia wewe uko na haki ya kusimama na kusema ya kwamba hizo nyumba zinafaa kupatiwa wananchi ambao wako katika Kaunti hii.

Nyumba zilizo hapa ziko pahali pazuri. Zilizojengwa Nyeri ziko kwenye uwanja pale Kieni. Tutakuta kwamba watu wetu wamepelekwa hapo wapewe za Nyeri nao watu walio Nyeri waletwe hapa, mahali ambapo ni pazuri na kuna maji, kisha watu wetu waende kuteseka huko. Sisi kama viongozi tunafaa kukataa katakata na kushika serikali koo kuhakikisha ya kwamba hawa wananchi wetu wamesaidika. Tukisema tunashika serikali koo sio eti tunaipiga, hapana. Lazima tusukume serikali ili isaidie mwananchi wetu ambaye alituchagua, ndio maana tumechaguliwa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba hawa Wabunge walio hapa tukubaliane na waniunge mkono kuwa wale wananchi walio hapa wapewe nafasi ya kwanza ya kupata hizo nyumba. Nataka kusikia kuna nyumba, Mheshimiwa Spika. Hata sisi hapa ni *mahustler.* Mimi ndiye *hustler* wa kwanza. Kama Ruto ndiye *hustler* wa kwanza basi mimi ndiye wa tatu kwa sababu Gachagua ndiye wa pili. Kutoka hapo, tunaenda kwa Shuel ambaye ndiye namba tano na Kamara ni wa sita, wako tu hapo katikati wakitafuta mambo ya *hustler.* Kwa hivyo, sisi ndio *mahustler* halisi na tunafaa kuwainua watu wetu kutoka chini hadi juu ile tuweze kusukuma lile gurudumu la *bottom-up*.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Kwa sababu sisi tuko na imani ya kwamba tutawasaidia watu wetu wa Laikipia Mashariki, nikimaanisha kila kona ya Laikipia, ningemwomba Mheshimiwa Muturi ambaye ni mmoja wa wale watu. Pamoja na watu wake, watakaofaidi kwa hizi nyumba, aniunge mkono na kuuafiki huu mswada ili tuhakikishe watu wetu wamepata nafasi ya kuuza vitu hapa. Yeye mwenyewe ni mwuzaji wa vifaa vya ujenzi. Tunataka kusikia yeye ndiye anasambaza misumari na saruji. Hata akisambaza ishirini pekee sisi tutafurahia kwa sababu tutajua pesa imebaki hapa kwetu. Kwa hayo machache, namwomba Mheshimiwa Muturi auafiki huu mswada. Asante.

Speaker: Hon. Mwaniki, the floor is yours.

Hon. Nicholas Mwaniki: Thank you, Mr. Speaker. I rise to second the motion that was tabled by Hon. Stephen. Having heard the motion on provision of affordable housing, the word affordable itself speaks very loudly to the Members of this Assembly, the whole county and the whole nation. The houses must be affordable. That is why, as you can see, there is provision of various types of houses in that section. We can see that there are sixty studio units, twenty-one-bedroom units, one hundred two-bedroom units, and twenty-three-bedroom units. As you can see, there is a good number of houses of various sizes and dimensions to cater for the needs of various types of people from various categories and economic statuses, so that we can be able as a government to provide housing for our people.

Many of our people are hustlers, and stating of hustlers, they are at the bottom when it comes to earnings and savings. So, a government coming up with such kind of a project to support the people who are downtrodden and cannot afford better houses is a viable thing. There is a partnership between the County and National Governments in order to support the electorate who elected us into the government, which is very crucial for the economy of our country.

These people who are being provided for by this government, it is not like they are not sober citizens of this nation. They are people who are of importance to this country and are the driving cogs of the economy no matter the status of their finances. Being able to provide them with housing so that they can live a better life in this Republic of Kenya is a step forward. I congratulate the National Government for having come up with this noble idea. Also, this housing project is a game changer in matters of business because, as you can see, we are supporting the micro, small and medium enterprises that are within our localities. We are building these houses in Nyahururu as well as in Nanyuki, and supporting our businesses is quite a noble idea.

Conducting business in this country is a little bit difficult today and doing business with these small-scale enterprises is key in driving the economy. We purchase materials from other counties or countries, yet we have manufacturers or small-scale traders who can distribute or supply the materials for building these houses. So, having a government supporting young people and small enterprises is key for the economy of Laikipia County, because we depend on the people of Laikipia for taxes and revenue collection in this county. Supporting them is a good idea, and as a government we are doing so in order to provide food on the table for the people doing business in this country.

Local manufacturers are also being taken care of as well as Jua kali artisans who will provide doors, windows and other necessary items that will be used for construction of these houses. The other people who have not been mentioned here are construction workers. As we can see, provision of labour is key in this country. Having a big population in this country yet being unable to provide work, this is a means of job creation. We may view it as short-term instead of long-term but these families will still be able to provide bread and pay school fees

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

for their kids. Having the skilled labourers to provide professional assistance in construction of these houses. Them being recruited in these projects, is quite a good idea which will support the economy of this county.

Mr. Speaker, I rise to second this motion because it is timely. As we move forward until the housing project is complete, I think the vetting of the people who will take over these houses should be done in a proper manner so that we can accommodate the neediest cases in this county and provide this basic commodity to our people of Laikipia. I rise to second. Thank you.

Speaker: Thank you, Hon. Stephen and Hon. Mwaniki.

(Question proposed)

Hon. Irene Wachuka: Asante Sana, Bwana Spika. Ninasimama kuunga mkono mjadala ambo umeletwa na Mheshimiwa Stephen Ndiritu *aka* Kagondu. Nashukuru sana serikali yetu ya Mheshimiwa wetu Rais wa Kenya William Samoe Arap Ruto na mdogo wake kwa maana waliketi chini na kufikiria mambo ya makaazi.

Nikikumbuka zile nyakati za baraza, kulikuwa na nyumba ambazo zilijengwa wakati ule. Nyumba hizo mpaka wa leo zinasaidia watu wengi sana. Ukienda Nyahururu, utapata makaazi inaitwa *Kiano Estate* ilifunguliwa na Waziri wa nyakati hizo Bwana Kiano wa Wanjiru.

Nyumba hizo ziko na vyumba viwili au vitatu vya kulala. Pesa ya kodisha wanayolipa haizidishi elfu nne mia tano. Kwa hivyo, naunga mkono na kusema tunatakiwa kama wananchi tuunge mkono mambo ya makaazi. Sio watu wote wana pahali pa kujenga wala sio watu wote wana nguvu ya kukodesha nyumba ya ghorofa ya vyumba sita vya kulala.

Serikali hii tulipokuwa tunawaomba kura, tulikuwa tunasema ni *bottom-up.* Kumaanisha kutoka chini na kuinua juu. Pesa mfukoni kwa yule Wanjiku mwenye yuko huko chini, mama mboga ambaye tulikuwa tunaomba kura tunamwambia alama yetu ni toroli. Wakati wa toroli kumlipa na kumjengea nyumba Wanjiku aliyeamka saa kumi na mbili kuenda kupiga kura imefika. Hata kama anauza mboga zake na makaa yake, atajua kuna kazi alifanya.

Pili, wakati mjadala inaletwa kama hii na huipendi, wacha siasa mingi. Usichangie wala usiunge mkono bali nyamaza. Kunao watu wengi sana ambao wanapinga mambo ya ujenzi wa nyumba za makaazi. Kama haujawahi kukodisha nyumba siku moja, basi hujui maana ya hizi nyumba zinazojengwa. Lakini, kama umewahi kukodisha nyumba ukaingia ukiwa na mtoto mmoja wakawa saba. Watoto wengine wakiwa wameoa, wengine kuoleka na wengine ambao hawajaoleka huku wakiwa na watoto wao.

Ninaunga mkono na kusema, kama vile hapa Nanyuki umeanzishwa ujenzi wa nyumba za makaazi, nangojea upande wa Nyahururu. Nyanja tayari ziko tatu Nyahururu za kujenga, sijui kama watajenga zote kwa umoja ama wataanza na moja. Kunayo kiwanja moja nilikuwa nabakisha ya ekari kumi na moja pia kuna ingine iko *Asian Quarters* ya ekari sita na bado kuna mahali ya ekari mbili unusu. Gavana pamoja na watu wake ndio watajua.

Wajumbe wenzangu, ngojeni tuunge mikono Serikali ya William Ruto kuhusu ujenzi wa nyumba. Wakati wa Mzee Kenyatta, hawakujenga nyumba za kukodesha, zilijengwa wakati wa Moi. Kuna makaazi kama Moi Estate, Kiano Estate na Starehe pahali nilikuwa naishi nikisoma.

Hata hapa, najua kuna zile nyumba za *kanjo* na zinasaidia watu wengi sana. Kwa hivyo, sisi kama viongozi wa mashinani tuliambiwa jana na Rais turudi mashinani tufanye kazi kama

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

timu moja na tumsaidie Wanjiku. Tuwache siasa mingi kwa sababu tulipewa nafasi ya kufanya kazi. Kazi yetu nikiwa mmoja ni kuunga mkono kazi ya Rais William Ruto.

Ninaunga mkono hadi na mali mjadala inapoletwa hapa. Ninaposikia kunatokea shida mahali fulani, kazi yangu ni kuwaita watu wa habari na kupigana na wale watu wanaosumbua serikali. Ngojeni tumpatie serikali nafasi. Wakati tulichaguliwa, hata sisi serikali haikuwa na kitu hata kwa hifadhi yake. Lakini, serikali imeanza kulipa kidogo kidogo hapa na pale juu lazima ushuru ya Kenya itarudi pale mahali ilikuwa.

Ninaunga mkono nikisema Waheshimiwa wenzangu, tuunge mkono serikali ya Ruto na mdogo wake Mheshimiwa Rigathi Gachagua. Kama ni Gavana, tumuunge mkono tukimwambia yote tunayotaka. Wale ambao tulikuwa Nairobi tuliona vile mambo yaliendelea na hata wewe Bwana Spika ulikuwa pale tukielewana kufanya kazi pamoja. Wakati wa vita hakuna kazi inaendelea.

Kama hutaki kufanya kazi, kaa nyumbani ama ukikuja hapa nyamaza. Usipinge kazi inayoendelea. Nikimuona Mheshimiwa Leshuel akiwa na mjadala na sitaki kuisikia, nanyamaza na upeane nafasi kwa wale wanaounga mkono. Kwa hivyo, ninaunga mkono na nitaendelea kuunga mkono kona yote ya serikali ya Rais William Samoe Arap Ruto na mdogo wake Mheshimiwa Rigathi Gachagua.

Kwa hayo machache na mengi, asanteni Wajumbe wenzangu. Ninamshukuru Bwana Spika, uliyenipeleka Nakuru nikasahau zawadi zote mbili; ningekuja nazo. Haikuwa kazi rahisi kwa kuwa hata sisi hatukujua ni nini inaendelea. Lakini nakushukuru, uliweka gari yako mafuta na kunipeleka. Asante.

Hon. Paul Leshuel: Thank you, Mr. Speaker. I want to thank Hon. Kagondu for this motion. I want to appreciate The Party Leader, His Excellency the President for calling the House to order so that he can support the motion of the Government.

I stand to support this because of three things. The affordable house apart from its own explanation, it also raises the economy of this county. There are so many people who are working there, supplying materials and others supply food. All those people who are working there must leave at the end of the day. The economy is doing well and everybody is benefiting.

Another thing, affordable house is very important because we all know that it is very hard to afford a house in this town. Therefore, when the Government gives you a chance to contribute slowly until you clear the balance, it is an opportunity to all Kenyans and luckily it is not about Laikipia only, it is countrywide.

Mr. Speaker, every Kenyan, a certain percentage will benefit but the challenge comes to our hands as leaders. What will be the criteria of giving affordable house to our people? But as we are leaders here, that is now our responsibility to make sure those people who are intended to be given are the beneficiaries such that we do not find that at end of the day the rich people who are owning bigger houses in this county become the beneficiaries of this thing. It is a national activity.

It is our responsibility as Members of this House to oversight and to see the smoothness of this project. This project must benefit the entire county of Laikipia because we are all tax payers, we are all Laikipians. I am not happy to hear somebody trying to narrow the speech or the agenda to our specific area. This is Laikipia, we must all benefit in all ways including job opportunities.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Mr. Speaker, the content of the motion is clear that this should benefit all of us as Laikipians. If possible, we are also happy to see ourselves being the employees or the casuals who are working there but obvious we know there is skill and capacity. There are so many things that might not give us the all chance to be there, but am sure the big percent is Laikipians.

It is good since it has come to this House when Nyahururu starts we need to come out so that all of us can bring our people. In this, they can get casuals from them because when they started building Nanyuki affordable houses, we did not take serious responsibility. The motion is very clear and we support the government of the day.

Mr. Speaker, if we don't support, unless we look for another government which can take us other five years. I am happy because some of the people were baptized yesterday and I am sure that majority of them will be the people who are supporting the government on the ground and not opposing the businesses of the government. I would like us to come up with a criterion in future that will give all of us an opportunity to get the affordable houses and the jobs as well. Thank you.

Hon. Mary Gathoni: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support the motion on provision of affordable housing. As we all know, the benefits of affordable housing is employment and dignified housing to all. The main worry is about employment. We have got welders and masons, young people and women who can do manual jobs around the site. How I wish that the locals should be engaged when it comes to that.

The other worry is transparency and accountability to ensure that every deserving Laikipian will benefit from the project. This will come when we come with a subsidized programme that will ensure that Laikipians gets the houses. Thank you.

Hon. Salim Edung: Bwana Spika, nashukuru. Nikiangalia kwa makini sana, katika sheria ya 2010, inaonyesha ya kwamba kila mtu anastahili kukaa katika nyumba nzuri. Ukiangalia katika nchi za nje, unakuta mambo ya nyumba ilifanywa kitambo. Kwa mfano nchi za Uarabuni. Sana sana huchukua watu kutoka Kenya na kuwapeleka huko. Ile kazi ambayo hufanya huko ni kazi ya manyumba. Hii inadhihirisha ya kwamba hili jambo la affordable housing lilianza kitambo.

Rais wetu alipotoa *manifesto* yake, alijua ya kwamba kuna watu ambao wameumia katika Kenya hii hasa wale ambao hukodisha manyumba. Unakuta mtu anakodisha nyumba elfu Hamsini au mia mbili. Lakini kwa sababu ya hii mikakati ambayo Rais ameweka kipao mbele, ili kupunguza gharama ya kwamba yule alikuwa akilipa elfu Hamsini, sasa ataweza kulipa elfu tano, itakuwa imepunguza zile pesa ambazo zingemsaidia kwa njia moja au nyingine kama kuelimisha Watoto.

Jambo lingine, katika hii mipango ya ujenzi wa manyumba, imeleta kazi nyingi. Unakuta inasemekana ya kwamba watu wamekosa kazi lakini sasa kazi imefika kwa sababu sasa zile nyumba hazitajengwa bila wafanyi kazi wa kibarua. Utapata vijana wengi wakifanya kibarua pale na kupata mapato yao ya kawaida lakini bila hizi nyumba, hakungekuwa na kazi. Pale kuna seremala na anapata kazi zingine kwa sababu yeye ni fundi wa mbao na pia mwashi anapata kazi ya mawe.

Ni lazima tuangalie mipangilio ambayo imeletwa na serikali kwa sababu imeletwa ili kusaidia Wakenya na kupunguza ukosefu wa kazi. Ninaona ya kwamba Mheshimiwa ambaye alileta huu mswada aliangalia mbali na katika wadi yake. pale Thingithu kuna vijana ambao wanafanya kazi hapo. Jioni wanapita huko kwa maduka wakinunua vitu kumaanisha ya kwamba baada ya kazi, anapita pale jioni akinunua kitu. Mimi ningeomba Wabunge wenzangu

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

waunge mkono kwa sababu hii *manifesto* tulikuwa tumeelezwa wakati wa kutafuta kura na Rais wetu. Tukiwa katika hili Bunge, tunashikilia hiyo *manifesto* ili itimike. Watu walikuwa wanadhania hizi ni heka heka za abunuwasi, kutaja lakini haifanyiki lakini sasa hivi katika Thingithu, sasa tunaoa hizo manyumba. Ningeomba Mheshimiwa Ndiritu kama kuna mikakati yoyote ameweka pale, aniangalie ili nipate nyumba mbili ili niweze kupunguza safari ya Kwenda Segera kila siku. Mungu awabariki.

Speaker: Thank you, Hon. Salim. Allow me to call upon the mover to make a reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika. Nasimama kujibu hata kama Mheshimiwa Shuel ananisukuma kama *wheel barrow* akaniambia nifanye haraka haraka. Mimi nilichaguliwa hapa kufanya kazi ili watu wa wadi yangu wasaidike. Nataka kushukuru Wajumbe wote ambao wamechangia na vile vile, kumshukuru Mheshimiwa Muturi kwa kuafiki huu mswada. Ni muhimu sana hasa huu wakati ambapo wananchi wetu wanahitaji nyumba.

Vile hawa Waheshimiwa wote wameweza kuchangia huu mswada, nimeona ya kwamba ni jambo la busara kuwa macho ili kuhakikisha ya kwamba wananchi wetu wamesaidika. Vile vile, nimesikia mwito wa Mheshimiwa Salim, Shuel na Kamara ambao hutoka mbali na wangetaka wawe na nyumba hapa na hilo ni jambo la busara. Ningetaka kusema ya kwamba katika Kaunti ya Laikipia, tuko na nyumba za serikali lakini utakuta ya kwamba wale ambao wanaishi huko sio wafanyi kazi wa serikali lakini ni watu wanalipa pesa kwa watu binafsi. Hizo nyumba zikaweza kupatiwa wale ambao hutoka mbali wakija hapa, inaweza kuwa ni jambo la busara maana hao ni wafanyi kazi wa serikali.

Katika hizi nyumba ambazo zinajengwa, nitaomba sisi wote tuungane na Idara husika katika kupatiana hizi nyumba. Mimi ninajua ya kwamba Idara ya Ujenzi na Mipangilio watakuwa kwa mstari wa mbele kuhakikisha ya kwamba nyumba zimepeanwa. Ningetaka sote tuwe mstari wa mbele kuhakikisha ya kwamba tumepata nyumba pale. Sisi pia ni watu wale ambao wako chini kwa sababu ukiangalia katika laini ya uongozi, sisi ndio tuko chini na tunafaa kushughulikiwa kama watu wako chini.

Sasa hivi, najua Mheshimiwa Salim akitoka hapa ataenda kutafuta nyumba mbali ili aweze kupata mahali pa kulala ili kesho aende Segera. Tukiwa na zile nyumba, atakuwa akifika hapo mapema na anakuja hapa mapema na pia akitaka kuondoka, anaondoka akitaka. Ningeomba hata Shuel pia apate nyumba hapa na sio kila wakati kupiga njia akielekea Mukogodo.

Ninajua vile kumekuwa na ukosefu wa usalama na yeye huwa anaongoza watu wengi na kuna wale ambao wana wivu na wanaweza kumshambulia, sisi hatutaki kuona mambo kama hayo. Hata yeye atapata na pia wale wengine wote lakini watapata kama sote tutaungana. Kama sisi hatutapata, hata yule mwananchi ambaye yuko huko chini atakuwa na shida. Kwa hivyo, naomba tushikane mkono na nimeshukuru vile Wajumbe wameona umuhimu wa huu mswada. Asante.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until tomorrow Wednesday, 13th March, 2024 at 9.00 a.m.

The House rose at 3.27 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*